Haifai kujidhuru wala kumdhuru mwingine

Kutoka kwa Abuu Saidi Sa'di bin Maaliki bin SInani Al-Khudry -radhi za Allah ziwe juu yake- yakwamba Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Haifai kujidhuru wala kumdhuru mwingine."

[Ni nzuri (Hasan)] [Imepokelewa na Ibnu Maajah, Daaruqutni na wengineo huku inafika kwa Mtume]

Amebainisha Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- kuwa ni lazima kuzuia madhara kwa aina zake zote na sababu zake zote kwako na kwa wengine, ni haramu kwa yeyote kujiudhi mwenyewe na mwingine kwa kiwango sawa. Na ni haramu kwake kukabiliana na madhara kwa madhara; kwa sababu madhara hayaondoshwi kwa madhara, isipokuwa kama itakua katika njia ya kulipiza kisasi pasina kuvuka mipaka.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/66531